



Tangazo la Kujisimamia

One Shared World ni shirika pana linalohusisha washikadau, matabaka, jamii, mashirika, makabila, tamaduni, matamania na mataifa mbalimbali kuhakikisha maisha mema ya usoni na utoshelezaji wa maisha mema ya kawaida kwa binadamu.

Tunapania kuinua demokrasia ya ubinadamu kama nguzo kuu duniani kuleta mabadiliko chanya katika maisha ya kawaida kuhakikisha maendeleo kufuatia kuweka wazi mahitaji yetu kwa jumla.

Kulingana na jinsi janga la COVID 19 limetuonyesha sasa kuwa sote ni sawa kwa kuwa tumehadhirika bila yeyote kusazwa. Tunashikilia kuwa:

Ushirikiano wetu sote unaweza kuwa kigezo cha kuwa na afya bora, amani na maisha mema ya usoni.

Kujukumika kwa usalama wetu wenyewe.

Usaidizi wa binadamu upo mikononi mwetu na malengo yetu yanatutegemea kuonekana wazi.

Nguvu wa umoja wetu hauwezi kutuzuia kujiendeleza wakati kunapokumbana na janga.

Hivyo One Shared World inaangalia matamania ya binadamu ya kawaida kwa misingi na haki za binadamu kikamilifu.

Ingawa mataifa yetu na mashirika duniani kote kwa sasa yamesimama kwa misingi ya kudumisha amani duniani, usalama na kadhalika bado hatujafikia lengo letu la kuweka wazi matamania yetu makuu ya kawaida.

Haya yanahusishwa ila sio kikamilifu:

- Kutokuwepo kwa uwezo wa kudhibiti msambao wa tauni kama COVID 19.
- Kushindwa kuzuia matokeo hatari kwa upana.
- Kutoweza kudhibiti makali yanayoadhiri hali ya hewa na mazingira kwa jumla duniani.
- Kushindwa kulinda watu wenye mahangahiko ya njaa kati ya makali mengine yakiwemo magonjwa.
- Ukosefu wa njia nzuri ya mawasiliano pamoja na uchumi mbaya.

Ugumu wa kupambana na changamoto hizi ni kutokana na kutoendana kwa vipaumbele vya nchi zetu na mahitaji yetu binadamu tunaotegemea sayari moja. Huku mataifa yetu yaliyopo na mashirika ya kimataifa kusalia imara. Tunaweza afikisha yote haya kwa kuungana mikono.

Kwa mujibu huu, tunapania kuunda nguzo ya tatu ya nguvu duniani zaidi ya mataifa na mashirika ya kimataifa yaliyotengenezwa na mataifa yetu. Nguzo hii inahusisha umoja duniani kote kwa misingi ya mahusiano na kisiasa kikamilifu.

Twaelewa kuwa nguvu ya maoni yetu binafsi kama binadamu lazima zitie moyo sio njia mbadala ya kazi ngumu inayotekelezwa na mtaifa mengi pamoja na mashirika ya kitaifa.

Tunataka viongozi wa mashirika haya wa viwango vyote kufanya maamuzi yatakayofaa matarajio ya nchi na duniani kwa manufaa ya watu wote.

Tunaamini mwendo wetu lazima ujengwe kwa misingi ya watu binafsi, mashirika na miungano yote duniani.

Tunashukuru ila teknolojia mpya husaidia kupata nafasi mzuri ya kuungana, watu ambao lazima wajiunge na mpango huu bado hawajapata mafasi ya kuwasiliana kwa njia hii ya mawasiliano.

Kutambua upana wa kauli hii ndiyo nguvu yetu, tunatangaza kuwa kujisimamia kote na mambo tunayofanya kwa ubinafsi Pamoja na watu wa jamii mbalimbali, mashirika na mataifa kwa jumla tupo pamoja.

Tunaahidi:

1. Kusaidia kuunda njia ya kudhibiti msambao kwa kutabiri, kuzuia na kutibu mashaka yanayotusibu.
2. Kusaidia wasiojiweza kuwa na hali nzuri ya maisha kama matajiri wanavyosaidika kwa kuwa maisha ni muhimu.
3. Kufanya kazi kwa pamoja kuhakikisha kila mmoja anafurahia kuishi kwa pamoja duniani.
4. Kufanya nchi salama kwa wanyama na viumbe wengine.
5. Kuhakikisha afya nzuri na usalama wa watoto wote pamoja na elimu bora kwa watu wote.
6. Kuunga mkono usanii ili kusaidia mawasiliano katika jamii mbalimbali.
7. Kushirikisha na kuinua kuabudu kwa binadamu kwa heshima na upole.

Kwa kuandikisha majina yetu tunajikatia shauri kujaribu kadri ya uwezo wetu kutimiza msimamo huu na kusihhi watu wote Pamoja na mashirika kuungana kuweka wazi mambo yanayotusibu kwa uwazi.

Hadi mwisho huu, sisi wazalendo wa mataifa mbalimbali na dunia tunayoshiriki twaahidi kwa kila mmoja nguvu ya maisha yetu nafasi ya bahati na heshima takatifu.